# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

## SALAMU ZA POLE



### Prof. Keto Elitabu Mshigeni

### 1944 – 2026



Mkuu wa Chuo, Baraza, Menejimenti na Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) tumepokea kwa huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Profesa Keto Elitabu Mshigeni kilichotokea tarehe 22 Machi 2026 katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete alipokuwa akipatiwa matibabu.

Profesa Mshigeni alizaliwa tarehe 14 Januari 1944 katika Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro. Alipata elimu yake ya msingi katika Shule ya Msingi Mpinji (1952 – 1955) na baadaye Shule ya Msingi Suji (1958 – 1959), kabla ya kuendelea na elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari Tabora (1960 – 1965). Alipata elimu yake ya juu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambako alihitimu Shahada ya Kwanza ya Sayansi mwaka 1969 kabla ya kuendelea na Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Chuo Kikuu cha Hawaii na kuhitimu mwaka 1974.

Profesa Mshigeni aliajiriwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1969 kama Mkufunzi Msaidizi na baadaye kupanda ngazi mbalimbali za kitaaluma hadi kufikia hadhi ya Profesa mwaka 1979. Katika kipindi cha utumishi wake chuoni, aliwahi kuwa Mkuu wa Idara ya Botania (1976–1982) na baadaye kuwa Mkurugenzi Mwanzilishi wa Kurugenzi ya Masomo ya Uzamili kuanzia mwaka 1980 hadi 1990. Kupitia nafasi hizi alitoa mchango mkubwa katika kuimarisha tafiti, kukuza ubora wa masomo ya uzamili na kuendeleza watafiti chipukizi.

Mbali na utumishi wake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Mshigeni pia alihudumu katika nafasi mbalimbali za uongozi wa kitaaluma kitaifa na kimataifa. Aliwahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, ambapo alichangia katika kuimarisha ubora wa elimu ya juu na tafiti katika taasisi hiyo.

Katika ngazi ya kimataifa, Profesa Mshigeni alitoa mchango mkubwa katika uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Namibia ambako alihudumu kama Naibu Makamu Mkuu wa Chuo wa kwanza anayeshughulikia Taaluma na Utafiti. Aidha, aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Tanzania Academy of Sciences (TAAS), Mhariri Mkuu wa jarida la Discovery and Innovation, pamoja na kuwa Mwenyekiti wa UNESCO/United Nations University (UNU)-Africa kwa ajili ya kuendeleza mpango wa Zero Emissions Research Initiative (ZERI) barani Afrika.

Profesa Mshigeni anakumbukwa kama mwanataaluma mahiri na mashuhuri aliyeta mchango mkubwa katika sayansi za botania, hususan tafiti za rasilimali za baharini hasa zao la mwani na uyoga, pamoja na kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali hizo kwa manufaa ya jamii.

Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Profesa Mshigeni katika maendeleo ya taaluma ya sayansi, utafiti na elimu ya juu, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kitaaluma barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Tunatoa pole za dhati kwa familia ya marehemu Profesa Keto Elitabu Mshigeni, ndugu, jamaa, marafiki, wanazuoni wenzake, pamoja na taasisi zote alizowahmi kuzihudumia na wote waliobahatika kufanya kazi na kujifunza kutoka kwake katika kipindi cha maisha yake yenye mafanikio makubwa.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**
**23 Machi 2026**